

MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TUME YA UTUMISHI WA UMMA: MAMLAKA ZA AJIRA NA NIDHAMU 90 ZAKAGULIWA

Imetolewa na Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma.

1.0 Utangulizi

Ndugu, msomaji Ijumaa ya wiki iliyopita tulipata fursa ya kusoma makala iliyoelezea jinsi Tume ya Utumishi wa Umma ilivyokamilisha kazi zilizoachwa na Tume zilizovunjwa baada ya kuanzishwa kwa Tume ya Utumishi wa Umma kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002. Tume hizo ni Tume ya Utumishi wa Walimu, Tume ya Utumishi wa Serikali za Mitaa na Tume ya Utumishi Serikalini. Katika makala hiyo tulielezwa kuwa kazi zilizokamilishwa na Tume ni pamoja na uthibitishwaji wa watumishi kazini, upandishwaji wa vyeo, ubadilishaji wa kazi na mashauri ya nidhamu na rufaa. Katika makala ya leo tutaangalia jinsi Tume ilivyotekeleza kazi ya ukaguzi katika mamlaka mbali mbali za ajira na nidhamu katika utumishi wa umma ambapo hadi Aprili, 2007 mamlaka za ajira na nidhamu 90 zilikuwa zimekaguliwa na Tume ya Utumishi wa Umma.

2.0 Ukaguzi wa mamlaka za ajira na nidhamu katika utumishi wa umma

Tume ya Utumishi wa Umma ina jukumu la kukagua mamlaka za ajira na nidhamu ili kuhakikisha kuwa mamlaka hizo zinazingatia kanuni na taratibu za kuajiri na kuchukua hatua za kinidhamu katika utumishi wa umma kwa lengo la kuboresha huduma zitolewazo na serikali kupitia utumishi unaozingatia sifa na usimamizi unaopima matokeo ya kazi. Kwa kuzingatia lengo hilo, kuanzia mwaka 2005/2006 hadi 2006/2007, Tume imefanya ukaguzi katika mamlaka za ajira na nidhamu 90.

Mamlaka zilizokaguliwa ni kama ifuatavyo:

- Wizara 23
- Idara zinazojitegemea 6
- Sekretarieti za Mikoa 21
- Mamlaka ya serikali za Mitaa 40

Maeneo yaliyokaguliwa na Tume ni ajira na nidhamu, likizo ya mwaka, likizo ya ugonjwa na upimaji wa wazi wa utendaji wa kazi na uthibitishwaji wa watumishi kazini.

3.0 Mamlaka zitakazokaguliwa na Tume kuanzia Julai 2007

Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Tume ya Utumishi wa Umma inatarajia kufanya ukaguzi katika mamlaka za ajira na nidhamu 74. Kati ya mamlaka 74, 69 zitakuwa Halmashauri za Wilaya, Manispaa, Majiji na Miji na mamlaka 5 zitakuwa Idara za Serikali zinazojitegemea. Maeneo ambayo yatafanyiwa ukaguzi ni ajira na nidhamu, Likizo ya mwaka, Likizo ya ugonjwa na upimaji wa wazi wa utendaji kazi(OPRAS). Tume inaziomba mamlaka zitakazokaguliwa kutoa ushirikiano wa hali ya juu ili kufanikisha kazi hiyo. Lengo kubwa la kufanya ukaguzi ni kuboresha huduma zitolewazo na serikali kwa kuhakikisha kuwa Wizara, Idara zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazingatia kikamilifu Sheria ya Utumishi wa Umma pamoja na kanuni na taratibu zake, miongozo na sekula zinazotolewa na Tume yenyewe pamoja na vyombo vingine vinavyohusika na masuala ya Menejimenti ya Rasilimali watu

4.0 Hitimisho

Tume ya Utumishi wa Umma iliundwa kwa Mujibu wa Sheria Na. 8 ya mwaka 2002 ili kuboresha Utumishi wa Umma. Aidha Tume ya Utumishi wa Umma ni chombo kinachoshughulikia usimamizi wa rasilimali watu, hivyo Tume ina jukumu la kufanya ukaguzi katika mamlaka za ajira na nidhamu ili kuhakikisha kama mamlaka hizo zinazingatia

ipasavyo sheria, kanuni na taratibu za ajira na nidhamu. Tunaziomba mamlaka za ajira na nidhamu kuongeza ushirikiano ili tuweze kufanya kazi kwa pamoja na kuikamilisha vizuri.

Ndugu, msomaji iwapo una maoni au ushauri tafadhali wasiliana nasi kwa anuani ifuatayo:

Katibu,
Ofisi ya Rais,
Tume ya Utumishi wa Umma,
S.L.P. 9143,
DAR ES SALAAM.
Simu: 022 – 2126811 - 4